



Vaccinator Training KAP Survey Fomu ya Ridhaa

Jina la Msimamizi Mkuu wa Mradi Tanzania: Dr. Henry Kiara
Jina la Taasisi: International Livestock Research Institute (ILRI)
Jina la Mfadhili: USAID – Feed the Future

Taarifa za Mradi na taarifa kuhusu mafunzo ya watoa huduma ya chanjo ya Ndigana kali

Mradi wa ITM2Scale unalenga kuongeza matumizi ya chanjo ya ugonjwa wa Ndigana kali nchini Tanzania kwa kutumia njia ya kuambukiza na kutibu (ITM), ili, kuondokana na matatizo makubwa zaidi katika kuboresha na kuimarisha uzalishaji wa mifugo katika nchi. Ili kutimiza azma hii, mradi unalenga kuongeza matumizi ya chanjo ya kuambukiza na kutibu, mradi utatambulisha na kuchunguza namna mbalimbali zitakazo wasaidia watoa huduma ya chanjo, wasambazaji na taasisi ama Wakala wa Serikali. Kwa wakati huu, mradi unaanzisha mafunzo ya watoa huduma ya chanjo ya ndigana kali kupitia wasambazaji. Lengo la mafunzo haya ni; kuongeza maarifa kuhusu ECF na chanjo ya kuambukiza na kutibi kwa watoa huduma, kuwahamasisha watoahuduma ili wapate mtizamo wa kibiashara katika utoaji chanjo na kuendeleza ujuzi kwa kuboresha mbinu za utoaji chanjo ya ndigana. Kutathmini maaendeleo, watoa huduma walio pokea mafunzo wanapaswa kujaza raundi kadhaa ya maswali ya utafiti kuhusu maarifa, mitazamo na mazoea yao katika utoaji wa chanjo. Taarifa hii itawajulisha wafanyakazi wa mradi, mswala ya mafunzo yaliyo na umuhimu zaidi na sehemu ambazo mafunzo yalikuwa na mafanikio zaidi. Pia data itachangia kutoa taarifa ya mradi kwa wafadhili.

Kabla hujaamua, unaweza kumuuliza muhusika yeyote mwenye uelewa ambaye unadhani anaweza kukueleweshwa kwa ufasaha kuhusu mradi na utafiti huu, na wewe ukamuelewa. Tafadhali uliza kama kuna mahali haujalewa vizuri ama ukihitaji ufafanuzi zaidi au kupata tafsiri ya maneno ambayo haujayeleva.

Ili utafiti huu uwe na manufaa, utaulizwa kujaza dodoso katika hafla tatu tofauti. Moja, kabla hujapokea mafunzo, pili, baada ya mafunzo na tatu, miezi kadha baada ya mafunzo. Maswali haya sio mtihani na utathmini hautafanywa kwa mtu binafsi ila kwa washiriki wote ambao watapokea mafunzo kijumla.

Taarifa zitakazokusanywa kutokana na utafiti huu zitatumika na kuhifadhiwa kwa umakini mkubwa. Taarifa zote zitakazo kuhusu zitakuwa katika mfumo wa namba badala ya jina lako. Ni watafiti peke yao ndio watakaojua namba yako, taarifa hizi zitatumizwa kwa usalama wa kutosha. Taarifa hizi hazitatolewa kwa watu wengine isipokuwa watafiti husika katika mradi huu. Baadhi ya taarifa ambazo haziwezi kuhusishwa na wewe zinaweza kuwekwa wazi kwa ajili ya kutumiwa katika tafiti zingine baada ya kipindi fulani kupita kama mfadhili wa mradi atakavyohitaji.

Uelewa tutakaopata kutokana na utafiti huu utarejeshwa kwenu kupitia utaratibu wa mawasiliano wa mradi kabla ya kusambazwa kwa umma na wadau wengine. Taarifa za siri hazitatolewa.

Ukitaka kujua zaidi kuhusu kamati hii ya maadili, mradi au taasisi ya ILRI tafadhali wasiliana na Dr. Henry Kiara (+254 720 412025) au Godfrey Bwana (+255 784600900).

Asante sana kwa kushirikiana nasi.